**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 24 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

24. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Moja kati ya lengo la kuweka taa za barabarani ni kupunguza ongezeko la ajali, vitendo vya uhalifu na kuufanya mji wetu kuvutia wakati wa usiku. Hata hivyo, changamoto kubwa ya taa hizi ikinyesha mvua kidogo tu au kipindi cha mvua nyingi, taa hizo huwa haziwaki na hata kipindi cha jua baadhi ya taa zinafifia mwanga wake na baadhi kutowaka kabisa.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuzikagua taa hizi na kuzifanyia marekebisho mara kwa mara.

(b) Je, wakati wa kufanya manunuzi, Wizara inajiridhishaje na ubora wa taa hizo ikiwemo uwezo wa betri zake, kutunza chanji, uwezo wa mwanga wake pamoja na uwezo wake wa kufanya kazi kwa muda mrefu.

(c) Serikali ina mpango gani wa kuendeleza uwekaji wa taa barabarani katika maeneo mengine ya mji wetu kama vile barabara ya Fuoni, Mwera, Fumba na kwengineko.

30. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa mara kadhaa tumeshuhudia kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar akielezea kutokuridhishwa na hali ya usafi wa mji wa Zanzibar. Pia hivi karibuni Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais katika ziara zake za kushtukiza amebainisha wazi kuendelea kukithiri kwa hali hiyo.

(a) Kuendelea kwa hali ya uchafu katika manispaa ya mji wa Zanzibar licha ya maagizo, makaripio na miongozo inayoendelea kutolewa na viongozi wakuu kila siku kunaleta tafsiri gani kwa wanaopewa maelekezo hayo.

(b) Ni ipi kauli ya Waziri husika kwa Mamlaka za Mikoa, Wilaya, Halmashauri na Manispaa ambazo ziko chini yake na ndio wenye dhamana ya kutekeleza.

(c) Kama haya yote yametokea katika kipindi cha jua kali, ni kipi wananchi wa Zanzibar watarajie kukiona katika kipindi kijacho cha mvua.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

104. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekeiti wa Baraza la Mapinduzi kuunda wizara ambayo inasimamia Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya watumishi kwamba wapo wafanyakazi wa Serikali wamekuwa wakikaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita hivyo kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma.

(a) Kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu ni lini itayashughulikia malalamiko hayo ya kukaimu kwa muda mrefu.

(b) Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kwamba nafasi za wafanyakazi hazijazwi hivyo kuleta ugumu wa utendaji. Je, ni lini Serikali itajaza mapengo hayo.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

69. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha huduma za afya katika vituo vyake mbali mbali vya afya. Hata hivyo, baadhi ya vituo hivyo kwa mfano Kivunge Cottage vinalalamikiwa kwa wagonjwa wanaolazwa kituoni hapo kukabiliwa na msongamano na masimbulizi hasa nyakati za usiku, hali hii inaonekana kuwa ni mikakati maalum.

Je, ni lini tatizo hili linatarajiwa kuondoshwa katika hospitali hiyo.

73. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali za kuboresha wodi za wagonjwa katika hospitali zetu Unguja na Pemba. Pamoja na jitahada hizo, wagonjwa wanaosumbuliwa na ugonjwa wa

kisukari wamekuwa wakipata shida sana hasa kwa wale ambao wanahudumiwa wakiwa na majeraha ya vidonda wanapokuwa kwenye mchanganyiko na baadhi ya wagonjwa pamoja na shida ya wananchi kuwanyanyapaa kutokana na athari za ugonjwa huu.

(a) Je, Serikali inafahamu kwa undani athari hizo na inatoa matumaini gani kwa binaadamu wenzetu wanaoathiriwa na ugonjwa huu ambao ni tishio katika kuboresha upatikanaji wa huduma.

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka daktari maalum wa matibabu ya ugonjwa wa kisukari katika Hospitali ya Micheweni ili kupata huduma ya uhakika.

(c) Je, ni lini Serikali itakuwa na wodi maalumu ya wagonjwa wa kisukari katika Hospitali ya Micheweni ambako kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa aina hii.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

17. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa muda mrefu mchezo pendwa wa mpira wa miguu Zanzibar umekuwa ukidorora hadi kufikia hatua ya kuwa na ligi kuu isiyo na mvuto na washabiki wengi wa soka kuacha kuhudhuria katika mechi za ligi hiyo. Kutokana na hali hiyo mashindano pekee ambayo yanapata watazamaji wengi ni ya ndondo na yale ya Mapinduzi CUP.

(a) Kwa kuwa mpira wa miguu ndio mchezo ambao unaongoza kwa washabiki wengi duniani. Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha hamasa za mchezo huo kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

(b) Kwa kuwa moja ya sababu kubwa ni kuanguka kwa mpira wa miguu Zanzibar ni ukosefu wa wadhamini na kwa kuwa msimu wa ligi kuu ya Zanzibar umefunguliwa tarehe 23/10/2021, ni mdhamini gani ambae atadhamini ligi hiyo na kiwango gani cha fedha.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

64. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada zake za kufuatilia matatizo ya maji kwa wananchi wake. Hata hivyo, utekelezaji wa kazi hiyo huwa mgumu kutokana na ukosefu wa miundombinu ya vifaa vya kuondosha tatizo la ukosefu wa maji Zanzibar.

Je, ni lini Serikali itaipatia Wizara hiyo miundombinu ya vifaa vya maji ili wananchi waepuke usumbufu wanaoupata wakati wanapohitaji huduma hizo.

138. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikitumia kisima cha chemchem cha Bungumi kwa kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Wilaya ya Wete wakiwemo wananchi wa jimbo la Pandani. Hata hivyo, kwa muda sasa, chemchem hiyo imetelekezwa na Serikali.

(a) Je, ni lini Serikali itaitengeneza barabara ya Machengwe-Kubwa kuelekea Bungumi kwenye kisima cha chemchem, ili vyombo vya moto na visivyo vya moto viweze kufika eneo hilo muhimu kama ilivyoahidiwa kwenye maelezo ya hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

(b) Je, ni lini Serikali itaidhibiti na kuiweka salama chemchem hiyo kwa kuiwekea mfuniko, mlango na mlinzi kama ilivyoahidiwa kwenye maelezo ya hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

(c) Je, ni kwa nini Serikali imekipuuza na kukitelekeza chanzo hicho muhimu cha maji kinyume na ahadi yake iliyotoa kwenye maelezo ya Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

128. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala wa Majengo inakusudia kutekeleza malengo ya kujenga nyumba mpya nane za Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni hatua ya awamu ya mwanzo ya ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Mawaziri zinazotarajiwa kujengwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

(a) Je, Wizara mpaka sasa imefikia hatua gani ya ujenzi huo.

(b) Je, ni nyumba ngapi mpaka sasa zimeshajengwa kati ya hizo nane.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

45. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaishukuru Serikali kwa kufanya matengenezo ya barabara ya dharura inapobidi. Imani yangu ni kuwa miradi yote huwa na kifungu cha bajeti.

Kwa nini mafundi wa matengenezo madogo madogo ya daraja la Machui, barabara ya Kiboje, Kizimbani na Mkokotoni hawajalipwa haki zao.

57. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya awamu ya nane kupitia kwenye ahadi zake Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Mwinyi alituahidi wananchi kutupunguzia shida ya ubovu wa barabara zetu za ndani kwenye majimbo yetu kwa kutujengea barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 200 kwa Zanzibar nzima.

(a) Je, Wizara inalijuwa suala hilo.

(b) Kama inalijua, Je, ujenzi huo unategemewa kuanza lini.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

125. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika malengo yake ya Bajeti ya mwaka 2021/2022, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ni kufanya ununuzi wa karafuu tani 7,000 na makonyo tani 1,200 na kuengeza uzalishaji katika mafuta ya mimea kwa kuimarisha mashamba yake pamoja na kuimarisha zaidi kiwanda cha mafuta ya makonyo na arki za mimea.

(a) Je, Wizara mpaka sasa imeshanunua tani ngapi za karafuu.

(b) Katika uimarishaji wa mafuta ya mimea, Je, ni kiasi gani kimeuzwa kwa msimu huu wa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

142. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kutambua hali za wananchi walio wengi, mwaka 1964, Serikali ilitangaza sera ya elimu bila ya malipo ili kusiwe na ubaguzi katika suala la kupata elimu kwa kadiri watoto wa wakulima na wafanyakazi watakavyoweza kusoma kwa upeo wa akili zao. Hata hivyo, kumekuwa na ubabaishaji katika utekelezaji wa sera hiyo kiasi kwamba wazee wanachangia kiasi cha lazima, kisichojulikana na kisicho kidogo kwa mwaka kwa jina la kuchangia gharama za elimu za watoto wao. Hii ni kuzikhalifu kimya kimya ahadi za viongozi wote wakuu wa Serikali.

(a) Je, Serikali imeidhinisha michango kwa ajili ya mambo ya Serikali kama vile karatasi za ofisi, mihuri ya ofisi, mitihani ya majaribio, manunuzi ya bendera ya Taifa, manunuzi ya picha za viongozi na mengineyo ili skuli ziweze kujiendesha.

(b) Je, ni upi msimamo wa Serikali kuhusu Sera ya Elimu Bila ya Malipo kwa sasa ukilinganisha na ile ya 1964.

(c) Je, ni lini Serikali itatoa waraka elekezi wa marekebisho ya Sera ya Elimu Bila ya Malipo mpya kama inavyotekelezwa sasa katika skuli zote za Serikali za Unguja na Pemba.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C):**

Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (P.A.C) ya Mwaka 2017/2018 na 2019/2020.

**Zanzibar,**
**24 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**